

MKATABA WA UPANGAJI

MKATABA huu umefanyika leo hii tarehe **01 Januari 2023**

KATI YA

CHIBANGO INVESTMENT COMPANY LIMITED wa S.L.P 22526 DAR ES SALAAM, (.....) (Ambaye katika mkataba huu atafahamika kama "**MWENYE NYUMBA**") kwa upande mmoja,

NA

AFRICAN BUSSINESS GLOBAL LIMITED wa S.L.P.....DAR ES SALAAM, (TIN) (Ambaye katika mkataba huu atafahamika kama "**MPANGAJI**") kwa upande wa pili.

KWA KUWA mwenye nyumba ni mmiliki wa nyumba na 31 iliyopo kwenye Kiwanja namba 24 Kitalu 37, Mtaa wa UDOE, Ilala, Dar es Salaam; NA

KWA KUWA mpangaji ana nia ya kupangisha OFISI kwa malipo ya kodi na masharti mengineyo yatakayoafikiwa kwenye mkataba huu

HIVYO BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIA YAFUATAYO:

1. Mkataba huu utadumu kwa miezi **THELATHINI NA SITA (MIAKA MITATU)** kuanzia tarehe **01 JANUARY 2023** na kumalizika tarehe **30 DISEMBA 2025**;
2. Kodi ya pango kwa MWEZI itakuwa ni **TSH 300,000/-** na italipwa kwa mikupuo **MITATU** ambapo utajumuisha kodi ya miezi **12**;
3. Kodi ya pango kwa mwaka itakuwa jumla ya **TSH 3,600,000/-**;
4. Mpangaji ataitumia OFISI hiyo kwa matumizi ya **kibiashara TU**.
5. **KWA UPANDE WAKE MPANGAJI ANAAHIDI YAFUATAYO:** -
 - (a) Kwamba hatasababisha uharibifu wowote katika OFISI. Iwapo Ikitokea uharibifu wowote, atawajibika kufanya matengenezo mara moja.
 - (b) Kwamba, mpangaji atawajibika kulipia gharama ya huduma (service charge) ambayo itajumuisha gharama ya ulinzi, umeme wa kwenye varanda/ngazi na usafi wa choo;
 - (c) kwamba, Mpangaji atawajibika kulipia umeme kwa mwezi anaoutumia katika Ofisi yake;


- (d) Kwamba, Mpangaji atawajibika kulipia kodi ya Ushuru wa Forodha (stamp Duty) ya mkataba huu;
- (e) Kwamba, mpangaji hatompangisha au kugawa NYUMBA kwa mtu mwingine yeyote bila ya ruhusa (idhini) ya Mwenye Nyumba.

6. KWA UPANDE WAKE MWENYE NYUMBA ANAKIRI YAFUATAYO:


- a) Kwamba lwapo mpangaji atalipa kodi ya pango ipasavyo na kutimiza masharti mengine yote yaliyoanishwa ndani ya Mkataba huu, basi Mwenye Nyumba au Mrithi au Mwakilishi wake hatambugudhi Mpangaji kwa namna yeyote ile.
 - b) Kwamba jukumu la kulipia kodi ya ardhi (land rent) na Kodi ya zuio ni juu yake.
7. Mkataba huu unaweza kuvunjwa kabla ya kuisha muda wake na upande wowote kwa kutoa taarifa ya siku 30 ya kusudio la kufanya kuvunja mkataba. Ikiwa ni Mpangaji ameamua kuvunja mkataba kabla ya muda wa mkataba huu kuisha basi kodi iliyokwisha lipwa haitarudishwa.
8. Mkataba huu unaweza kuhuhishwa tena (**RENEWABLE**) baada ya kumalizika muda wake kwa makubaliano mapya kati ya mpangaji na Mwenye Nyumba

KWA USHUHUDA na UTHIBITISHO, mkataba huu umewekwa sahihi na Mwenye Nyumba na Mpangaji kama inavyoonyeshwa hapa chini:


MKATABA huu umesainiwa hapa **Dar es salaam Na CHIBANGO INVESTMENT COMPANY** ambaye ninamfahamu binafsi mbele yangu leo hii tarehe.....01.....mwezi.....03.....2023

MBELE YANGU


KAMISHNA WA VIAPO/WAKILI
MKATABA huu umesainiwa hapa **Dar es salaam na ABC LIMITED** ambaye ninamfahamu binafsi mbele yangu leo hii tarehe...01...mwezi.....03.....2023

MBELE YANGU


KAMISHNA WA VIAPO/WAKILI





MWENYE NYUMBA



36100/-
 9984208246466
 22/03/2023
